# K.C.S.E 2008 KISWAHILI (102/3)
## MWONGOZO WA KUSAHIHISHIA - FASIHI
## KARATASI YA 3

For more free KCSE Revision Papers and Answers visit http://www.joshuaarimi.com

I a). i). Wanajamii wanajishughulisha katika kazi mbalimbali ili kuboresha maisha yao lakini maisha yao ni duni

ii). Vibarua (manamba, wachapakazi, mayaya, madobi, matopasi) wanaoajiriwa wanafanya kazi kwa bidii lakini mishahara yao ni duni

iii). Viongozi serikalini wamepewa nyadhifa hizo za hadhi lakini hawajibiki kunyanyua hali za waliowachagua

iv). Tabaka la chini ndio walio wengi katika jamii na ndio tegemeo la jamii lakini wanaishi maisha ya mateso mengi

v). haijulikani mateso ya walio wengi yatafika kikomo lini *zozote 4 x 1 = alama 4*

b). i). Kinaya

ii). Wasakatonge ndio wengi lakini hawana sauti

iii). Makuli, mayaya, matopasi, wachapakazi n.k ni maskini

iv). Wasakatonge wafanyao kazi kwa mateso mishahara yao ni duni

v). Wapelekao watu serikalini hawashughulikiwi na waliowachagua

vi). Wazalishao mali hawana chochote bado ni maskini (manamba, madobi, mayaya, wachapakazi)

II i). Taswira

ii). Wabeba zege ya marashani

iii). Wasukuma mkokoteni

iv). Makuli bandarini

v). Wachimbaji migodini

vi). Manamba mashambani

vii). Wachapakazi viwandani

viii) Matopasi wa majaani

ix) Wanasiasa madarakani

x) Mayaya na madobi wa nyumbani

(siku zote wako matesoni)

III i). Takriri

ii). Wasokatonge

iii). Juakali

iv). Lakini

v). Wao

vi). Ni

IV. i). Ulingunuzi/ ulinganushi

ii). Wachimbaji migodini lakini maisha – yao ni ya chini

iii). Wachapakazi viwandani lakini maskini

c). i). Kipande kimoja

ii). Shairi lina kituo/ kimalizio

iii). Mizani hailingani katika kila ubeti

iv). beti 4

v). Mishororo 6 kila ubeti / tasdisa / usita au kila ubeti una kichwa au kijichwa / anwani na kila ubeti una mishororo mitano



Connect with Joshua Arimi in facebook
For Tips on passing KCSE register @ http://www.joshuaarimi.com

vi). Mshororo wa kwanza vina vinabadilika ( li na – nge)
vii). Mshororo mitano ina vina vinavyofanana (ni)
viii). Mshororo wa kwanza katika kila ubeti unapindapinda ( pindu)
ix). Neno lakini limetumiwa mwanzo wa kila kituo – kikwamba

d). watu wa tabaka la chini / ndio huwapa nyadhifa viongozi / kutokana na nyadhifa hizo viongozi hupata mali au uwezo wa kiuchumi / wale waliowachagua maisha yao ni ya kusikitisha

e). i). Kufanya kazi kwa bidii
ii). Kuwajibika – kwa umma katika kushiriki kuwachagua viongozi
iii). viongozi wanastahili kuadilika kwa kunyanyua hali za umma na kujali hali ya wafanyikazi

f). Manamba – vibarua, wafanyikazi tabaka lisilo auheni – watu maskini / wasio na hali nzuri kiuchumi/ walalahoi

i). Maelezo ya sauti kuhusu uwezo mkubwa wa jua ambao mtemi hawezi kunyanyasa au kutesa. Uwezo wa jua unaashiria uwezo wa umma ambao utamwangamiza Bokono. Amekuwa ana uwezo wa kufanya mambo mengi lakini uwezo wa jua unaashiria kwamba umma una uwezo utakaomzidi Bokon na kumuongoa mamlakana
ii). Kutokuwepo kwa watu katika mkutano ni dalili kwamba watamuasi hatimaye. Watu hawakuwa na imani na uongozi wa Bokono kwani walikuwa wamechoswa nao
iii). Ndoto ya Bokono kuhusu kuzikwa kwake akiwa hai ni ishara ya kuangamizwa kwake na utawala wake. Ndoto inaonyesha dalili kuwa ingawa bokono angali hai wanabutangi hawamtaki
iv). Tendo la kushika mkia wa mjusi/ nyoka anayemuuma na kumwachia sumu ni ishara ya matokeo na hatari ya kuchezea haki za wananchi. Bokono kupuuza upinzani wa wanabutangi kwani haamini uongozi wake una hitilafu
v). Ndoto ya Tanya ya samba aliyelaa kando ya kisima ni ishara ya kiongozi anaywewazuia watu kufaidi rasilmali ya umma na uhuru. Bokono na uongozi wake umehodhi mali na kuwazua wanabutangi uhuru wa kufaidi nayo,
vi). Ndoto ya pili ya Tanya kuhusu kichwa kinachobadili na kuwa na sura ya mwelusi ni mdokezo wa ishara ya mwelusi anayeuwa na nduguye Gege
viii) Masimulizi ya aski kuhusu kisa cha Makea aliyelelewa hoi na kuwa nusu maiti huku akichekelewa na jua ni ishara ya kiongozi anayepagawa na kulewa mamlaka anavyofanya Bokono Hatima ya uhai (maiti ya mjusi) inaashiria kikomo cha ungozi wa Bokono
ix). Nyalwe kutoa picha ya Bokono kurudi tumboni mwa mamake inaashiria mwisho wa utawala na Bokono

a).
i). Katika kisima cha mkomani/ Bonde la ila ngi
ii. Msemaji ni zigu mojawapo wa washauri
iii). Anazungumza na kaloo
iv). Kaloo angependa kumshukuru mtemi kwa sababu aliamuru mwanawe apewe kazi/ alitaka kumshukuru zigu kwa kuzungumza na mtemi juu ya mtoto wake akapata kazi

b).
i). Ni watu wa kuitikia kila kitu anachosema mtemi
ii). Waemlimbikizia kiongozi wao sifa zisizo za ukweli k.v mtukufu, Baba wa Butangi n.k
iii). Wanadai kuwa mungu amempa Bokono utawa
iv). Wanamsifu kwa kuongoza kwa busara kwa manufaa ya wote- walio karibu naye ndio waliofaidi



For more free KCSE Revision Papers and Answers visit
http://www.joshuaarimi.com
Connect with Joshua Arimi in facebook
For Tips on passing KCSE register @ http://www.joshuaarimi.com

v). Wanamhimiza atawale kwa miaka 100 – Haiwezekani
vi). Wamsifu kwa uvumilivu – anatisha kutafuna mifupa yao
vii). Wanakumbusha kuwa Bokona anawashauri watu kuishi kwa amani na umoja ingawa si kweli – vita vya kikabila
vii). Hawamwambii ukweli / hali ilivyo – mkutano unaposusiwa wanasema watu watakuja
viii). Licha ya kame kuwa mshauri anageuka na kujiunga na wanabutangi

i). Wanawake hasa wazee hawakujua kusoma na kuandika
ii). Wanawake wanajihusisha na biashara ndodo (bi keti) wanafanya biashara maarufi ni wanaume – selele
iii). Wanawake wanakumbwa na umaskini – Bi keti
iv). Wanawake wanahimizwa kufanya kazi Fulani kv. Kusomesha said anamshauri muna
v). Wanaume ndio wanaoamua mambo kuhusu posa kv said, salimu, bushiri na selele
vi). Mwanamume ndiye aliyekuwa na hadhi kuu – ndiye anayelisha na kuvisha anyanyua yale yanayopita nje katika ulimwengu
vii). Udhibiti wa wanaume – salimu anasisitiza kuwa hasani ana haki ya kutenda analotaka
viii). Mwanamke alitakiwa kuficha udhodari wake – muna na kazi yake
ix). Maswali ya watoto – chuo kikuu – kushunghuliwa na waume
x). Wanaume wanaweza kungiliana na watu wengine bila jamii kuwashuku lakini sivyo kwa wanawake – uonika na Rashid
xi). Hatuoni wanawake wenye vyeo
xii). Monika anaishia kuolewa na mtu asiye na elimu ya juu
xiii). Tajiri kama Bi Maryamu hashughhulika na maendeleo
ix). Asha kupewa nafasi inayoendeleza uongo na uharibifu
iix). Salama ni msomii na mfanyikazi lakini hakui kama mhusika anakaa kumsubiri Rashid amuoe
iiix). Katika maswala ya kisheria wanawake hawajimudu Bi. Keti anasaidiwa na mhaji na Bi. Maryamu anasaidiwa na Hamisi

a). Makosa ya Ali
i). Tangu utotoni alikuwa mgomvi na kulikuwa na matatizo mengi baina yake na walimu
ii). Alizozana na watoto wa majirani pale nyumbani
iii). Alipoingia chuo kikuu alijihusisha na mambo mengine kama siasa
iv) Alipenda anasa na alikuwa na marafiki wengi wa kike
v) Ingawa alikuwa hodari mahudhurio yake katika mijadala hayakuwa mazuri na mtihani ulipofika alijikuta hajajiandaa.
vi) Alikubali ushawishi wa kutumia dawa.
vii) Ali daima hakuzingatia mawaidha ya wasimamizi wa chuo na anakataa kurekebika
viii) Wasimamizi wa chuo walimwita babake azungumze na Ali na pia hakubadilika.
ix) Alikataa kukiri na kufichua aliyemuuzia vidonge.

**Mwisho wa kosa**
Alipofukuzwa chuo kikuu alijisaka nafsi yake na kujirekebisha

**Makosa ya Asha**
i). ALimwonea wivu Bi. Keti
ii). Alimchukia keti kwa uzuri wake
iii). alikuwa mwenye kiburi – alinuna aliposhiriwa kutoka ili mamake aseme na keti



For more free KCSE Revision Papers and Answers visit http://www.joshuaarimi.com
Connect with Joshua Arimi in facebook
For Tips on passing KCSE register @ http://www.joshuaarimi.com

iv). ALibadilisha vyombo vya dhahabu alivyoazima keti
v). Alimsingizia keti na kufungua mashtaka
vi). Alikuwa mwongo – alikuja kukaa kwa mamake kwa kisingizio wamekosana na mumewe
vii). Asha aliiba vyombo vya dhahabu
viii). Asha hakufurahia makubaliano baina ya mamake na keti jinsi ya kulipia vyombo – ukatili alitaka Bi keti aumie
ix). Kuficha tabia mbaya za mumewe

**Mwisho wa kosa**
Makosa haya yote yalibainika inapofichuliwa na inspekta Hamisi kuwa Asha aliungama kosa kuwa ndiye aliyevichukua vyombo

**PWAGUZI**

a). i). Sheikh kijuba na waumini wengine walimwamini Salimu kuwa ni mwalimu mzuri wa dini . aliwalaghai wakampa pesa nyingi – anatoweka na kuwaibia
ii). Kijuba – anapokea pesa za sadaka na chana kuzitumia kwa manufaa yake

b). **PUMBO**
i). Makulu anaaminiwa na kupendwa na watu anawapa vijana bangi
ii). Andanda adhaniwa ni mlozi kumbe sivyo

c). **MSAMARIA MWEMA**
Kizito kibambo kudhaniwa anamtadarukia
Likono kumbe ndiye aliyemgonga

d). **SIKU YA MGANGA**
Wagonjwa wanadhani daktari (Mwaibale ni gwiji kumbe sivyo )

e). **UTEUZI WA MOYONI**
i). Mzee saidi amwoza Bintiye kwa furaha akidhani ametokea mume mzuri kumbe sivyo
ii). Uchaguzi – waliyemchagua wakidhani atawasaidia hakuwafaa

f). **NGOME YA NAFSI**
Watu wanafikiri Naseko amekuwa bibi lakini anafaulu kutoroka

g). **KACHUKUA HATUA NYINGINE**
i). Binti maritu kupachikwa mamba na mtu ambaye tungetaraji amlinde
ii). Mwajiri wa mavitu kumpa mikopo akidhamiria kumpokonya ardhi

h). **TUZO**
Kibwana anaamini anaenda kupokea tuzo anajitayarisha lakini mwishowe anapewa Salome

i). **MAYAI WAZIRI WA MARADHI**
i). Waziri anaomba maradhi ya kipindupindu ili idadi ya watu ipungue
ii). Mayai alimpenda mwanawe ukombozi sana lakini anaporejea kama mzuka anawakashifu viongozi kama babake

j). **MKIMBIZI**
Vita vya kikabila vilipozuka kati ya wahutu na watutsi haikuaminika kwa kuwa watu hawa walikuwa wameishi kama majirani na ndugu lakini wanageukana na kuuaua.



For more free KCSE Revision Papers and Answers visit http://www.joshuaarimi.com
Connect with Joshua Arimi in facebook
For Tips on passing KCSE register @ http://www.joshuaarimi.com